# HUDUMA YA KUTEMMBELEA

WACHUNGAJI, WAZEE NA MASHEMASI

Kutembelea nyumba kwa nyumba ni kwa muhimu kwa wote achungaji na washiriki. Washiriki wanahitaji kujua kuwa wachungaji na wazee wao wanajali.Wachungaji na wazee nao wanahitaji kujua washiriki wao wanaishije katikati ya juma na ni shida au matatizo gani yamewasibu.

**Huduma ya Kutembelea wakati wa Agano la Kale na Jipya**

Licha ya uelewa mfinyu wa baadhi ya wachungaji juu ya mpango wa kutembelea, msingi wa kutembelea nyumba kwa nyumba ni wa kibiblia. Mungu mwenyewe alitembelea watu wake kabla na baada ya anguko la dhambi. Ukweli ni kwamba Mungu mwenyewe ndiye aliyechukua hatua ya kuwatafuta angalia (Mwanzo 3:8,9)

Maandiko hayaelezi kwamba Mungu wetu ni Mungu anayeogofya na kutisha bali niMungu wa upendo anayependa watoto wake na anayewatembelea soma Mwanzo (18:1-10)

Hata hivyo Mungu baba alifanya zaidi sio kutembelea tu, Ili kufahamu tatizo la watu wake na uchungu wa dhambi Mungu alimtuma kabisa mwana wake apate kukaa nao aelewe matatizo yao apate kuwasaidia kuwaoko katika shida zao. Vilevile alikuja ili awe kielelezo (Yohana 1:14)

Katika huduma yake Yesu aliwahurumia watu, aliwatembelea,a kiwasaidia katika maisha yao ya kiroho na kuponya magonjwa yao (Marko 5:35-43, Luka 19:5)

## Maandalizi Ya Kutembelea

Wewe kama kiongozi andaa na weka mazingira yako ya kiroho vizuri kwa njia ya kutenga muda wa kusoma neno, kuomba na kujitakasa.

Utakumbuka kuwa unapotembelea unaenda kuendesha ibada kila nyumba hivyo unapaswa uandae mahubiri mengi mafupi ya fungu moja au mawili yenye lengo la kuongoa mshiriki atoke hatua moja hadi nyingine.

Hebu sikia roho ya unabii inavyosema kwa watu wanaojaribiwa kuhubiri bila wao wenyewe kusoma;

# Umuhimu na Faida ya Huduma ya Kutembembelea

Unapotembelea washiriki unagundua mambo mengi

a. Utagundua shida zao
b. Mapungufu yao
c. Matatizo yao ya kiroho
d. Itakurahisishia kujua maeneo ya kupalilia na maeneo maeneo ya kutengeneza na kutoa ushauri wa kiroho mapema

Nyumbani au mahali pa faragha ndipo washiriki wako wanapoweza kuwa huru kueleza wazi shida zao na kuwasaidia na sio kwenye mikutano ya pamoja.Faida nyingine ya kutembelea ya huduma ya kutembelea ni kwambwa itakusaidia kujenga joto la kiroho,kukuza mahusiano na washiriki huko wakijenga matumaini kwa huduma kwa viongozi wao.

Baadhi ya viongozi wanadai hawana nafasi kwa kwa sababu ya shughuli nyingi za kazi. Kiasi kwamba hawana muda wada wa kutembelea. Ndugu John Sutherland anatumia usemi huu kupinga hilo "Ni kosa kubwa kudhani kwamba huduma ya mtu mmoja mmoja (kutembelea) ni tofauti na kazi na wajibu wa kichungaji wa kila siku…"[1]

Mama White anasisitiza umuhimu wa kiongozi kutembelea anasema " Kumbuka kwamba kazi ya mchungaji haiishii kuhubiri mimbarani kwa kuwafungulia watu maandiko matakatifu tu. Yeye ambae ni mwaminifu kwa kazi yake nje ya mimbari atakamilisha kazi yake mara kumi zaidi kuliko kazi ya anayekaa mezani " [2]

## Mikakati na mbinu za Kutembelea

Ili ufanikiwe katika kazi ya uchungaji haya yafuatayo yanaweza kusaidia maendeleo ya kazi yako kanisani au mtaani kwako.

1. Mara tu unapohamia mtaa mpya au unapochaguliwa kuwa mzee wakanisa tembelea nyumba zote za washiriki wako hilo litakusaidia kuwathibitishia kuwa unawajali. Baada ya hapo kama wewe ni mchungaji au mzee wa kanisa utawashirikisha wazee, mashemasi hata na watendakazi wengine wa Kanisa kutembelea washiriki mara kwa mara
2. Wewe kama kiongozi wa Kanisa au mtaa katika kutembelea sehemu kubwa shughulika na haya makundi maalum kama vile wagonjwa, wenye huzuni,

[1] John Sutherland Bonnell, *Psychology for Pastor and People* (New York: Harper & Brothers, 1948), p. 8.
[2] White. *Testimony for the Church vol 9.(*Hagerstown, Maryland: R&H Graphics, 1947) 124

3. ndoa changa, ndoa zenye mataizo, wazazi wapya,wazazi wenye watoto nyumbani. Viongozi wengine wapange kutembelea washiriki wote kila robo
4. Wafundishe na kuwatia moyo wakumbushe washiriki kuwasiliana na Kanisa wanapokuwa na matatizo wape washiriki namba zako za mawasiliano waweke huru kwa muda na wakati wanapoweza kuita mchungaji,mzee au shemasi – hasa wakati wa matukio makubwa kwa mfano **kabla ya kwenda hospitali, wakati mototo anapozaliwa,wakati msiba unapotokea,au kunapokuwa na simanzi au majonzi ya muda mrefu,kabla mshiriki hajakata tama, ndoa yake haijaharibika, kabla anguko la kiroho halijamkumba au unamjua mtu fulani aliye hitaji la kiroho.**
5. Wakati mwingine unaweza kutembelea washiriki kwa njia ya simu hiyo nayo ni kama nusu ya kuonana.
6. Weka mazingira yafaayo ya kupatikana kanisani wakati ukiwa ofisini au wahi nusu saa mapema siku ya sabato kabla shule ya sabato kuanza kutakuwa na watu kutia moyo watakaokuja. Hii itakupunguzia gharama za kutembelea.

**Mwisho**

Huduma ya kutembelea sio huduma ya muda fulani tu au huduma ya ziada kwa majukumu ya kiongozi la bali huduma hii na ichukuliwe kama sehemu muhimu ya huduma ya kiongozi.Unapotembelea mashauri na huduma ya maombi ni ya muhimu na ihusishe watu wote wa familia husika waadventista na hata wasio waadventista.

Na

Pr Joseph Lusega

Ministerial and Family Life NETC